SHULE YA SEKONDARI TUKUYU

S.L.P. 27

Barua pepe ……………………………

Mob - 0768858548 AU 0763455191

Tarehe ……………………

Kumb Na. ……………………………………………………

Jina la mwanafunzi …………………………………………

………………………………………………………………

S.L.P. ………………………………………………………

………………………………………………………………

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU WILAYA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2021**

1 : 0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I Katika Shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari **TUKUYU** ipo umbali wa km 0.5 Kutoka Halmashauri ya **WILAYA YA RUNGWE**

Muhula wa kuanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba.

2 : 0 **Mambo muhimu ya kuzingatia.**

2: 1 **Sare za Shule**

**KWA WAVULANA**

1**. Suruari mbili**. (i) Moja rangi ya bluu nyeusi (dark blue) kitambaa cha “Cotton”
(ii) Ya pili rangi ya damu ya mzee kitambaa cha “Cotton”.

2. **Shati mbili:** nyeupe zenye mikono mifupi tetroni.
3 . **Viatu vyeusi** vya kamba visivyo na kisigino kirefu.

4. **Soksi nyeupe na ndefu jozi mbili.**
5. Sweta ya rangi ya kijani kibichi shingo yake iwe na umbo la V – (Mzazi anunue mwenyewe)
6. Suruali zote mbili zinashonwa na mzazi. Angalia kiambatanisho.

**KWA WASICHANA**

1**.Sketi mbili ndefu(sketi fupi haitapokelewa)**

(i) Moja rangi ya blue nyeusi (dark blue)
(ii) Rangi ya damu ya Mzee

2. **Shati mbili nyeupe** zenye mikono mifupi tetroni
3. **Soksi nyeupe ndefu** Jozi mbili
4. **Viatu vyeusi** visivyo na kisigino kirefu vya kamba
5. Sweta ya rangi ya kijani kibichi shingo yake iwe na umbo la V. (Mzazi anunue mwenyewe).

. Watakao hitaji kuvaa hijabu wanatakiwa kuvaa sketi ya rangi ya bluu na damu ya Mzee ndefu inayotosha kusetiri mwili wa atakaye vaa. (rangi ya hijabu ni nyeupe).

## 2 : 2 VIFAA VYA MASOMO

Unatakiwa kuleta vifaa vya masomo kama ifuatavyo:-

- Madaftari makubwa (caunter books) kwa masomo yote 11 atakayosoma.(Quire 3)
- Kalamu za wino (bluu na nyeusi)
- Kalamu ya risasi
- Mkebe wa Hisabati (Mathematical Set).
- Kamusi ya Kiingereza (dictionary) na vitabu vya masomo husika.

**Vifaa vingine vitakavyokaguliwa wakati wa kuripoti ni:**

**i)** Jembe moja lenye mpini (**kwa wavulana**) na mopa moja
**ii)** Kwanja moja (**kwa wasichana**) na draya moja.

**VIFAA VYA MICHEZO WAVULANA:**

- Tracksuit rangi ya blue bahari.
- Raba jozi moja.
- Fulana (T-sheti)rangi nyekundu damu mzee na soksi ndefu rangi ya blue.

**WASICHANA :**

- Tracksuit rangi ya blue bahari
- Raba jozi moja,
- Flana (T-sheti)rangi nyekundu damu ya mzee

## 2 : 3 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya **Elimu Na. 25** ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais **- TAMISEMI** yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.:

a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation) binafsi.

d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa.

e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule.

g) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote na

h) Kutunza mali za umma.

2 : 4 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule.

a) Wizi

b) Uasherati

c) Ubakaji

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine mirungi, kubeli na kadhalika.

e) Kupigana au kupiga.

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g) Kudharau Bendera ya Taifa.

h) Kupata mimba/kusababisha mimba.

i) Kuoa au kuolewa

j) Kutoa mimba.

k) Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

m) Kumiliki simu ya mkononi maeneo ya shule.

n) Kuruka uzio wa Shule.

3 : 0 **Mambo Mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni na mwanafunzi:-**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na Sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

## NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU

…………………………

**MWL FRANCIS MWAKIHABA**
**MKUU WA SHULE**

**Kiambata Na.3**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKINOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**
**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**
**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:**

**SEHEMU A:**

1. Jina kamili la mwanafunzi ---------------------------------------------------------------------------

2. Tarehe ya kuzaliwa ----------------------------------------- kabila ---------------------------------

3. Jina la mzazi/mlezi ------------------------------------------------------------------------------------

4. Uhusiano ------------------------------------------ kazi yake ------------------------------------------

5. Anuani ya Mzazi/Mlezi ------------------------------------------------------------------------------

6. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ---------------------------------------------------------------------

7. Umbali kuja Shuleni ni KM ---------------------------------------------------------------------------
8. Majina ya Ndugu/Walezi wengine wa karibu;-

| JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU | MAHALI ALIPO |
|---|---|---|---|
| (i) | | | |
| (ii) | | | |
| (iii) | | | |
| (iv) | | | |

**TANIBIHI:** Wale wenye picha tu.

9. **<u>MENGINEYO:</u>**
(Kama mgonjwa aje na uthibitisho wa daktari, kama ni yatima aje na hati ya kifo, kama ni mlemavu, n.k).
**-----------------------------------------------------------------------------------------------------------**
**-----------------------------------------------------------------------------------------------------------**

## SEHEMU B:
## TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:

Mimi ---------------------------------------------------------------------- (majina matatu) nimezisoma na kuzielewa Sheria, Kanuni na Taratibu za Shule na kwamba niko tayari/ siko tayari kuzifuata.

Sahihi ya mwanafunzi --------------------------------------- Tarehe --------------------------------------------

## SEHEMU C:
## TAMKO / AHADI YA MZAZI/ MLEZI:

Mimi --------------------------------------------------------------- ambaye ni Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi ----------------------------------------------------------- ninaahidi kwamba nitatekeleza maagizo na mahitaji yote muhimu ya Shule kama nilivyoelekezwa na kwamba niko tayari kushirikiana na Uongozi wa Shule katika suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu ili kuinua taaluma na nidhamu yake. Pia ninakubali kutii Taratibu, Kanuni na sheria zote za shule na kulipa michango kama ilivyoelezwa pia nitafuata maelekezo mengine kadri yatakavyotolewa na uongozi wa Shule ya Sekondari Tukuyu.

Sahihi ya Mzazi / Mlezi ------------------------------------------------ Tarehe --------------------------------